KATIBA YA BARAZA LA TAIFA LA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI TANZANIA (NACOPHA)

Chapisho la January 2013

KATIBA
YA BARAZA LA TAIFA LA WATU WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI TANZANIA
National Council of People Living with HIV (NACOPHA)

Chapisho la January 2013

YALIYOMO

VIFUPISHO VYA MANENO 4

DIBAJI 5

Kifungu 1.0 FASIRI 7

Kifungu 2.0 JINA LA BARAZA 8

3.0 : Dira, Dhamira, Lengo na Madhumuni 9

3.1: Dira 9

3.2 : Dhamira 9

3.3. Lengo kuu 9

3.4 Madhumuni 9

SURA YA NNE 11

4.0 UANACHAMA WA BARAZA NA MASHARTI YA UANACHAMA 11

4.1 MASHARTI YA UANACHAMA 11

4.1.1 HAKI YA MWANACHAMA 11

4.1.2. WAJIBU WA MWANACHAMA 11

4.2 HADHI NA UHUSIANO WA BARAZA NA MITANDAO YA WATU WANAOISHI NA VVU 12

Kifungu 5.0 Uwakilishi katika Baraza 13

5.1: Sifa za Mwakilishi 13

Kifungu 5.2 Wajibu na Haki ya Mwakilishi. 13

5.3 UKOMO WA UWAKILISHI 14

Kifungu 6.0 Muundo na Uongozi wa Baraza la Watu Wanaoishi na VVU 15

6.1. Mkutano mkuu wa Baraza. 15

6.1.2 Kazi na majukumu ya Mkutano mkuu wa Baraza 16

6.2 Bodi ya Uongozi 16

6.2.1 Kazi na majukumu ya Bodi ya Uongozi 17

6.2.2 Sifa za mjumbe wa Bodi ya Uongozi. 18

6.3 Sekretarieti 18

6.3.1 Wajibu na majukumu ya Sekretarieti; 18

6.4 Konga 19

6.4.1 Muundo wa Konga. 19

Kifungu 7.0: MAJUKUMU NA WAJIBU WA VIONGOZI WA BARAZA. 21
7.1. MWENYEKITI 21
7.1.1 Madaraka na wajibu wa Mwenyekiti *21*
7.2 Makamu Mwenyekiti 21
7.2.1 Madaraka na wajibu wa Makamu Mwenyekiti *21*
7.3 Afisa Mtendaji mkuu. 22
7.3.1 Madaraka na wajibu wa Afisa Mtendaji mkuu *22*
7.4 Mweka Hazina. 22
7.5 Viongozi wa konga 23
7.5.1 Mwenyekiti wa Konga *24*
7.5.2 Makamu wa Mwenyekiti wa Konga *24*
7.5.3 Katibu wa Konga *24*
SURA YA NANE 26
Kifungu 8.0: Fedha za Baraza. 26
8.1 Vyanzo Vya Fedha 26
8.2 Taratibu za Fedha. 26
8.3 Matumizi ya fedha na Ukaguzi wa Mahesabu ya Baraza. 27
SURA YA TISA 28
Kifungu 9.0. MALI NA DHIMA YA BARAZA 28
10.0. MAREKEBISHO YA KATIBA, USULUHISHI WA MIGOGORO NA KUVUNJWA KWA BARAZA 29
10.1. MAREKEBISHO YA KATIBA 29
10.2 KUVUNJIKA KWA BARAZA LA WATU WANAOISHI NA VVU 29
10.3 . USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDANI YA BARAZA 29
Kifungu 11.0 : MAELEZO MENGINEYO 30
11.1. MUHURI NA NEMBO YA BARAZA 30
11.2 NEMBO YA BARAZA 30
SURA YA KUMI NA MBILI 31
12.0 : Marekebisho ya katiba ya NACOPHA ya mwaka 2005 31

VIFUPISHO VYA MANENO

CMAC	Council Multisectoral AIDS Committee
GIPA	Greater Involvement of People Living with HIV and AIDS
HIV	Human Immuno Virus
MIPA	Meaningful Involvement of People Living with HIV/AIDS
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania
NACOPHA	National Council of People Living with HIV
NGOs	Non Governmental Organizations
NMSF	National Multi-sectoral Framework
TNCM	Tanzania National Coordinating Mechanism
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VMAC	Village Multisectoral AIDS Committee
VVU	Virusi Vya Ukimwi
WMAC	Ward Multisectoral AIDS Committee

KATIBA YA BARAZA LA TAIFA LA WATUWANAOISHI NA VVU (NACOPHA)

DIBAJI

Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) Tanzania, linaundwa baada ya kutafakari na kuridhika kuwa kuna umuhimu wa kuwa na chombo kimoja cha kitaifa cha kuratibu masuala yote yanayohusu watu wanaoishi na VVU Tanzania

Azimio la kuanzishwa kwa chombo hiki lilifikiwa na wawakilishi wa Watu wanaoishi na VVU nchini katika kikao kilichofanyika Hoteli ya Land Mark Ubungo-Dar es salaam tarehe 25 hadi 27 Agosti 2003.

Baraza la taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania, litahakikisha na kuweka msukumo katika kuratibu na kusimamia uwezeshaji, tiba, mafunzo na misaada kwa watu wanaoishi na VVU Tanzania

Aidha Watu wanaoishi na VVU ni jamii iliyo katika hatari ya kudhulumiwa haki zao kwa visingizio mbalimbali vikiwemo :

(i) Changamoto za kiafya

(ii)Kutokuwa na uwezo wa kushiriki katika shughuli za Kijamii, kiuchumi na Kisiasa

(iii)Unyanyapaa na ubaguzi unatokana na hali ya kuishi na VVU

(iv) Kutokuwa na uelewa au uelewa mdogo wa masuala yanayohusu haki za binadamu.

(v)Mapungufu yanayojitokeza katika uhamasishaji, mafunzo tiba na Usaidizi.

Hizi ni baadhi tu ya changamoto ambazo huchangia kutuathiri kimazingira, hali ambayo inahatarisha maisha ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI

Hivyo kwa ;

Kutambua juhudi za serikali ya Tanzania katika kutunga sera na mikakati ya mapambano dhidi ya VVU katika jamii yetu.

Kudhukuru haki za Binadamu ikiwa ni dhana ya msingi kwa maendeleo ya jamii, hususani watu wanaoishi na VVU katika jamii yetu,

Kutambua kuwa kutokuwepo kwa Baraza la uratibu la watu wanaoishi na VVU ni dhahiri kunadhoofisha nguvu ya ushawishi wa Watu wanaoishi na VVU katika kutunga Sera na Programu mbalimbali za kudhibiti UKIMWI nchini.

Kutafakari, kanuni ya ushiriki thabiti wa watu wanaoishi na VVU (GIPA Principle) iliyotamkwa na wakuu wa nchi mbali mbali katika mkutano ulifanyika mwaka 1994, Paris Ufaransa ambayo inaelekeza ubia katika shughuli za kudhibiti UKIMWI katika nchi husika,

Kudhihirisha kuwa, watu wanaoishi na VVU na wengineo wasioishi na VVU wanayo dhamana kubwa, wajibu na majukumu ya kuzuia kuenea kwa maambukizi mapya ya VVU, mafunzo na Usaidizi.

Kuzingatia Tamko rasmi la baraza kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao maalum (UNGASS) kuhusu VVU kuanzia tarehe 25-27 Juni, mwaka 2001, lililotolewa na wakuu wa nchi.

Wajumbe, Wawakilishi wa Watu wanaoishi na VVU, wa jinsi zote kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa kwa Tanzania tuliokusanyika katika Hoteli ya Travetine, Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 30 Machi hadi 01 Aprili 2005, baada ya kupitia na kupitisha katiba tunaazimia kuunda Baraza la Taifa la watu wanaoishi na VVU Tanzania ;National Council of People Living with HIV/AIDS(NACOPHA)

1
SURA YA KWANZA

Kifungu 1.0 FASIRI

Kwa mujibu wa katiba hii na kwa kuzingatia muktadha wa maneno yaliyotumika, misingi na madhumuni ya Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU Tanzania (NACOPHA), dhana na maneno yanayotumika katika Katiba hii yatakuwa na maana halisi, kama yalivyoainishwa na kutafsiriwa hapa chini kwa mujibu wa katiba hii na si vinginevyo.

VVU: linaainisha kifupi cha ' 'Virusi vya UKIMWI :

UKIMWI : Linaainisha Upungufu wa Kinga Mwilini.

Baraza la Taifa : Ni chombo cha juu kabisa cha taifa cha usimamizi na uratibu wa masuala na shughuli za Watu wanaoishi na VVU Tanzania.

Mtandao : Ni chombo au vyombo ambavyo vitatumika na Baraza na wadau katika kutekeleza program za UKIMWI kwa watu wanaoishi na VVU.

Bodi ya Uongozi: Ni chombo kinachoongoza na kusimamia shughuli za Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU **.**

Sekretarieti : Ni chombo cha utendaji wa kila siku wa shughuli/kazi Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU

Walengwa : Ni watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI**.**

Kanuni/Masharti : Ni taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha uendeshaji na usimamizi mzuri wa shughuli za Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU

Fedha/Hazina : Ni fedha na mali zozote zitakazopatikana kutoka ndani au nje ya Baraza

Konga: Ni chombo cha juu ndani ya Halmashauri husika cha usimamizi na uratibu wa masuala na shughuli za Watu wanaoishi na VVU

GIPA (Greater Involvement of people Living with HIV)/**MIPA** (Meaningful Involvement of People Living with HIV) : Ni Makubaliano ya kimataifa ya Ushirikishwaji wa dhati wa Watu wanaoishi na VVU**.**

Kifungu 2.0 JINA LA BARAZA

2.1 Linaanzishwa Baraza huru kwa mujibu wa Sheria 'the Societies (Application for registration) Rules 1954 iliyotungwa kwa mujibu wa the Societies Act (Chapter 337 Revised Edition 2002), kwa mtazamo wa mashirikiano bila kujihushisha na masuala ya kisiasa, kidini au shughuli zozote kinyume cha katiba hii na sheria ya Asasi zisizo za Kiserikali ambalo litajulikana kama NATIONAL COUNCIL OF PEOPLE LIVING WITH HIV/AIDS (NACOPHA) kwa tafsiri ya kiswahili litajulikana kama Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU kwa Tanzania

2.2 Shughuli za Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU zitaendeshwa Makao Makuu au sehemu nyingine Tanzania kwa mujibu wa Katiba na kwa kuzingatia sheria za nchi.

2.3 Anuani ya Baraza la taifa la watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, itakuwa ni

NATIONAL COUNCIL OF PEOPLE LIVING WITH HIV/AIDS (NACOPHA)
S.L.P 55811 Dar es Salaam ; Tanzania
Simu +255 22 2701210 Nukushi. +255 22 2701209
Barua pepe: nacopha@nacopha.or.tz,
Tovuti www.nacopha .or.tz

2.4 : Hadhi ya kisheria

Baraza la taifa la Watu wanaoishi na VVU (NACOPHA) litakuwa ni shirika lisilo la kiserikali, kisiasa, kidini na lisiloendeshwa kibiashara.

Litakuwa shirika linalojitegemea, la kudumu na litakuwa na muhuri wake.

Kifungu 2.5 : Lugha rasmi

Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU, litaendesha shughuli zake kwa kutumia lugha ya Kiswahili na au Kiingereza kama lugha rasmi za mawasiliano. Itakapobidi lugha nyinginezo za kimataifa zitatumika kwa manufaa ya Baraza , na kila zinapotumika mkalimani atatumika.

SURA YA TATU

3.0 : Dira, Dhamira, Lengo na Madhumuni

3.1: Dira

Kuwa na Taifa ambalo watu wanaoishi na VVU wanaishi kwa kuheshimiwa na kufurahia mahitaji ya msingi na haki za binadamu

3.2 : Dhamira

Kuunganisha, kutetea na kuratibu juhudi za vikundi, mashirika na mitandao ya watu wanaoishi na VVU zinazolenga kuwa na jamii nzuri yenye maisha bora.

3.3. Lengo kuu

Lengo kuu la Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU ni kuleta pamoja watu wanaoishi na VVU, kuratibu juhudi, ushiriki na ushawishi wao katika mapambano dhidi ya UKIMWI. Hii ni pamoja na kutimiza malengo na madhumuni yafuatayo:

3.4 Madhumuni

3.4.i Kuwezesha muungano na umoja wa Watu wanaoishi na VVU katika kubuni, kupanga na kutekeleza programu na mipango funganishi ya Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU

3.4.ii : Kutetea utekelezaji wa Haki za Binadamu kwa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

3.4.iii: Kutetea nafasi ya watu wanaoishi na VVU kwa lengo la kuleta uwiano wa maendeleo kama mbinu ya kupunguza kiwango cha umasikini na kudhibiti kuenea kwa maambukizo ya VVU ndani ya jamii.

3.4. iv: Kuimarisha mafunzo, tiba na juhudi za uwezeshaji zinazopatikana ndani ya jamii.

3.4. v Kuwezesha ufahamu wa jamii kuhusu malengo na madhumuni ya Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU kwa njia ya semina, Kongamano, warsha na vikundi vya majadiliano na sanaa katika ngazi zote kuanzia jamii hadi Taifa

3.4.vi . Kushirikiana na Serikali na wadau wengine walio na azma dira na ragba sawa na Baraza la watu wanaoishi na VVU, kitaifa na kimataifa.

3.4.vii Kukuza, na kuwezesha uanzishwaji wa mitandao baina ya wadau wote kitaifa na kimataifa, kwa lengo la kubadilishana habari na kushirikiana matumizi ya rasilimali zilizopo ili kuendeleza hali za maisha ya watu wanaoishi na VVU nchini Tanzania.

3.4. viii Kupiga vita unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU kama njia ya kuendeleza na kuimarisha amani upendo na mshikamano ndani ya jamii kupitia teknolojia ya mawasiliano, elimu na habari

3.4. ix Kujenga uwezo wa taasisi za watu wanaoishi na VVU ili waweze kusaidia mtu mmoja mmoja na au familia za watu wanaoishi na VVU kupitia program zao

3.4. x Kuendeleza utendaji haki ndani ya jamii kwa kushiriki mchakato wa kuleta mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni kwa kuzingatia misingi ya tabia, mila, na desturi.

3.4.xi Kuandaa mikakati ya kushawishi na kuendeleza mchakato wa kidemokrasia kwa lengo la kuimarisha uwakilishi wa watu wanaoishi na VVU kama njia ya kuleta mabadiliko ya mahusiano ya kibinadamu ndani ya jamii.

3.4.xii Kuwasiliana kwa karibu na Konga za watu wanaoishi na VVU katika masuala yote yenye lengo la kufanikisha na au kutimiza azma, dira na madhumuini ya Baraza kwa mujibu wa katiba

SURA YA NNE

4.0 UANACHAMA WA BARAZA NA MASHARTI YA UANACHAMA

Mwanachama wa Baraza la Taifa la watu wanaoishi na VVU ni mtu yeyote aliyetambuliwa kuwa anaishi na VVU na kuratibiwa kupitia kwenye Konga na Mitandao na aliye tayari kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa na katiba hii

4.1 MASHARTI YA UANACHAMA

i. Awe ni mtu aliye huru na wazi kuhusu hali yake ya kuishi na VVU
ii. Kujaza fomu na kutambuliwa na uongozi wa Konga au Mitandao ya watu wanaoishi na VVU
iii. Awe amelipa kiingilio na ada za uanachama kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa na Katiba hii
iv. Awe tayari kushiriki pamoja na watu wanaoishi na VVU katika shughuli zilizokubaliwa na Konga au Mitandao kwa madhumuni ya maendeleo na ustawi wa watu wanaoishi na VVU
v. Awe tayari kujitoa na kujitolea kwa shughuli za Baraza, Konga na mitandao mahali popote nchini

4.1.1 HAKI YA MWANACHAMA

i. Kuchagua na kuchaguliwa kuwa kiongozi katika baraza
ii. Kushiriki na kutoa maoni ya kujenga chombo hiki katika vikao mbalimbali vinavyomuhusu
iii. Kushiriki katika shughuli zote za Baraza kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa na katiba hii.
iv. Kulindwa na kutetewa katika kudai haki yake ya msingi dhidi ya chombo kingine kilicho nje au ndani ya mfumo wa Baraza
v. Kupata taarifa mbalimbali za Baraza kulingana na utaratibu wa upatikanaji wa taarifa hizo ambazo anastahili kupata mwanachama

4.1.2. WAJIBU WA MWANACHAMA

i. Kuhudhuria vikao vyote vinavyompasa kama ilivyoainishwa kwenye katiba hii
ii. Kutotoa siri za Baraza nje ya Baraza kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa na Baraza
iii. Kulipa ada zake kwa muda unaostahili ili baraza liweze kujiendesha

bila vikwazo

iv. Kutoa taarifa na maoni yake kwa kufuata taratibu zilizowekwa katika ngazi husika inayohusu baraza kwa manufaa ya watu wanaoishi na VVU.

v. Kujitoa na kujitolea katika kushiriki shughuli za Baraza na vyombo vyake.

4.2 HADHI NA UHUSIANO WA BARAZA NA MITANDAO YA WATU WANAOISHI NA VVU

i. Baraza litatambua mchango wa mitandao ya watu wanaoishi na VVU katika ngazi zote kama vyombo vya utekelezaji wa program za mwitikio kuhusu UKIMWI nchini.

ii. Kwa kuwa mitandao hiyo ina dira, dhamira zake, kwa mujibu wa katiba zao, mitandao hiyo itangia maridhiano na Baraza (Memorundum of Understanding -MoU) kama wabia wa utekelezaji wa program za UKIMWI. Kila upande husika utawajibika kuheshimu maridhiano hayo.

iii. Mitandao hiyo itatafsiriwa na kanuni zitakazowekwa na katiba hii

Kifungu 5.0 Uwakilishi katika Baraza

Kutakuwa na Uwakilishi wa WAVIU wa aina kuu mbili ambao kulingana na vigezo vitakavyowekwa watachaguliwa ama watateliwa kulingana na taratibu na miongozo iliyowekwa. Wawakilishi hawa watakuwa kama ifuatavyo:

5.a. Wawakilishi wa watu wanaoishi na VVU ndani ya Baraza katika ngazi zote (Kijiji/Mtaa, Kata, Halmashauri za wilaya, miji,manispaa, na jiji hadi vikao vya kitaifa

5.b. Wawakilishi wa watu wanaoishi na VVU katika vyombo vilivyo nje ya Baraza (kama vile TNCM, NMSF, MKUKUTA, Technical Working Groups,CMACs, WMACs,VMACs, mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa na vinginevyo vitakavyojitokeza)**.**

Wawakilishi katika kundi **a** na **b** ni lazima kuzingatia usawa wa jinsia na au kanuni, taratibu na vigezo vitakavyotolewa na chombo au ngazi husika

5.1: Sifa za Mwakilishi

i. Awe raia mzawa wa Tanzania na anayetambuliwa na Konga au mitandao ya watu wanaoishi na VVU
ii. Awe na taaluma stahiki kama itahitajika kulingana na nafasi ya uwakilishi anaouomba au kuteuliwa kulingana na miongozo itakayokuwepo
iii. Awe anaishi na VVU na awe wazi na hali yake ya kuishi na VVU
iv. Awe na utayari wa kuwakilisha watu wanaoishi na VVU kwa nafasi atakayochaguliwa au kuteuliwa nayo
v. Awe na ari ya kujitolea katika shughuli za Baraza/Konga/Mitandao na vikundi vya watu wanaoishi na VVU
vi. Awe na akili timamu.

Kifungu 5.2 Wajibu na Haki ya Mwakilishi.

Mwakilishi yeyote kama ilivyoiainishwa katika ibara ya 5 a na b anao wajibu wa:

a. Kuhudhuria na kutoa maoni ya kujenga chombo hiki katika vikao mbalimbali na kutoa mrejesho kwa maandishi kwa chombo au ngazi husika, kupiga kura, kuchagua viongozi na kuchaguliwa kushika nafasi ya uongozi.

b. Kuwa tayari kwa wito wowote na kwa wakati wowote anapohitajika kwa shughuli za Baraza.
c. Kutoa taarifa zozote zitakazohitajika na Baraza toka kwake kwa manufaa ya Baraza
d. Kupendana na kuheshimiana kwa dhati na Wawakilishi wenzake na Watu wanaoishi na VVU bila kujali jinsia, rangi, kabila, dini au itikadi za kisiasa.
e. Kushiriki katika shughuli zote za Baraza kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa katiba hii.
f. Mwakilishi ataruhusiwa kupata taarifa muhimu za Baraza katika ngazi husika kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizopo
g. Mwakilishi atakuwa na haki na jukumu la kutetea maslahi ya Watu Wanaoishi na VVU katika ngazi au chombo husika
h. Mwakilishi anayo haki ya kulindwa na kutetewa na Baraza kwa jambo lolote litakalotokana na uwakilishi wake kwa manufaa ya Baraza

5.3 UKOMO WA UWAKILISHI

a. Kujiuzulu uwakilishi kwa sababu yoyote ile baada ya kutoa taarifa kwa maandishi kwa ngazi husika ya kufanya hivyo katika kipindi kisichopungua siku tisini **(90)**
b. Kutenda kosa kwa mujibu wa vyombo husika na au kitendo chochote cha kuhujumu Baraza .Hatua hii itapitishwa kwa kuthibitishwa na vikao mbalimbali vya ngazi husika
c. Kushindwa kuhudhuria vikao husika vitatu mfululizo bila sababu ya msingi na kutotoa taarifa rasmi ya maandishi
d. Kujihusisha na vitendo vilivyo kinyume na madhumuni ya baraza, katiba ya Baraza na sheria za nchi,ambavyo vinaweza kuleta athari kwa Baraza na Taifa kwa ujumla.
e. kufukuzwa na Baraza kutokana na utovu wa nidhamu .Hatua hii haitachukuliwa mpaka kwanza mtuhumiwa amepewa nafasi ya kutoa utetezi wake mbele ya vikao husika na vikao kuridhika kwa kupitisha azimio hilo kwa theluthi mbili(**2/3)** ya kura za wajumbe waliohudhuria vikao hivyo kwa mujibu wa taratibu na kanuni zilizopo.
f. Kutokuhudhuria vikao mfululizo kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa sababu za kiafya
g. Kutokuwa na akili timamu baada ya kuthibitishwa na daktari
h. Kifo

SURA YA SITA

Kifungu 6.0 Muundo na Uongozi wa Baraza la Watu Wanaoishi na VVU

Usimamizi na uongozi wa Baraza utafanyika chini ya Muundo na ngazi za maamuzi zifuatazo:

(i) Mkutano mkuu wa Baraza
(ii) Bodi ya Uongozi
(iii) Sekretarieti ya Baraza
(iv) Konga ya Halmashauri husika

6.1. Mkutano mkuu wa Baraza.

Kutakuwa na Mkutano mkuu wa Baraza utakaoandaliwa na kuitishwa na Bodi ya Uongozi.

(i) Mkutano mkuu wa Baraza utakuwa ndicho chombo cha juu kabisa cha maamuzi na Uongozi.
(ii) Utahudhuriwa na wajumbe wote wa Bodi ya Uongozi wa Baraza waliopo madarakani, wawakilishi wawili kutoka kila mtandao wa kitaifa, mwakilishi mmoja kutoka makundi maalum, wenyeviti wa Konga na mwakilishi mmoja kutoka kila konga.Ikiwa mwenyekiti wa Konga atakuwa **Me,** basi mwakilishi atakuwa **Ke** au kinyume chake
(iii) Utaitishwa kila mwaka na itakapobidi Mkutano mkuu maalumu wa Baraza utaitishwa kwa jambo maalumu wakati wowote. Na baada ya miaka mitatu utaitishwa mkutano mkuu ukiwa na ajenda mojawapo ya Uchaguzi mkuu
(iv) Taarifa ya Mkutano itatolewa si chini ya siku tisini (90) na agenda za Mkutano kutumwa kwa Wajumbe kabla ya tarehe ya mkutano
(v) Taarifa itatolewa siku thelathini (30) kabla ya tarehe ya Mkutano endapo wito wa kwanza haukufanikiwa
(vi) Utafanyika katika wito wa tatu kwa 1/3 ya idadi ya Wajumbe endapo miito miwili haikufanikiwa, baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Baraza
(vii) Aidha unaweza kuitishwa mkutano mkuu wa Baraza maalum na Bodi ya uongozi kwa jambo maalum. Taarifa ya Mkutano mkuu wa Baraza maalum itatolewa kwa Wajumbe katika kipindi kisichopungua siku ishirini na nane (28) kabla ya tarehe ya mkutano

(viii) Mahudhurio ya Mkutano mkuu wa Baraza maalum yatakuwa si chini ya 2/3 ya wajumbe wote waliosajiliwa kwa mujibu wa katiba hii.

(ix) Ombi la kuitishwa mkutano mkuu wa Baraza maalum laweza kuletwa kwa maandishi kwa Bodi ya Uongozi na Wajumbe endapo litaungwa mkono na wajumbe wasiopungua 1/3 ya wajumbe wote wa mkutano mkuu wa Baraza.

(x) Mkutano Mkuu wa Baraza Maalum utafanyika katika kipindi kisichozidi siku ishirini na nane (28) toka ombi lilipowasilishwa

6.1.2 Kazi na majukumu ya Mkutano mkuu wa Baraza

Mkutano mkuu wa Baraza ukiwa ndiyo ngazi ya juu kabisa ya maamuzi utafanya kazi na kutekeleza majukumu yafuatayo.

(i) Kupokea, kupitia na kupitisha sera mbali mbali za Baraza la Watu wanaoishi na VVU.

(ii) Kujadili na kupitisha katiba ya Baraza na au marekebisho yake.

(iii) Kuchagua na kuthibitisha viongozi wa Baraza ikihusisha nafasi ya Mwenyekiti, Makamu wa mwenyekiti, Mweka hazina na Wajumbe wa Bodi ya uongozi ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi ya Uongozi itakapotokea kuwa wazi.

(iv) Kupokea na kuidhinisha, Mipango, Bajeti za miradi na taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za Baraza

(v) Kupokea taarifa ya mkaguzi wa nje wa mali za Baraza

(vi) Kupitisha jina la mkaguzi wa nje wa Hesabu za Baraza baada ya Bodi kupendekeza wakishauriwa na Sekretarieti

6.2 Bodi ya Uongozi

Kutakuwa na Bodi ya Uongozi wa Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU itakayochaguliwa na Mkutano mkuu wa Baraza yenye Wajumbe wasiopungua saba (7) (Ikizingatiwa kuwa ni idadi ya chini) na wasiozidi kumi na tatu (13) ikiwa ni idadi, ya juu) wajumbe kumi wa kuchaguliwa, na 3 wataalamu.

Bodi ya Uongozi itajumuisha makundi yafuatayo:

i. Mweyekiti, Makamu Mwenyekiti na Mweka Hazina waliochaguliwa na mkutano mkuu wa Baraza

ii. Mwanamke mmoja mwenye sifa ya uongozi anayeishi na VVU atakayetokana na jukwaa la wanawake wanaoishi na VVU

iii. Vijana wawili (me na ke) wenye sifa za uongozi wanaoishi na VVU (Umri kati ya miaka 18-29) watakaotokana na jukwaa la vijana wanaoishi na VVU

iv. Wajumbe wanne watakaopatikana kwa mujibu wa kanuni zitakaozowekwa na katiba hii.
v. Waataalamu wasiozidi watatu; kipaumbele kiwe kwa watu wanaoishi na VVU na angalau mmojawapo awe mwanamke

Wajumbe wa Bodi ya uongozi watachaguliwa kwa kufuata utaratibu ama mfumo ufuatao:

i. Majina ya wajumbe wa Bodi ya Uongozi ambao ni wataalam yatapatikana kwa kuombwa kupitia mapendekezo ya Sekretariati kupitia kwenye Bodi ya Uongozi na kuthibitishwa na Mkutano mkuu wa Baraza.
ii. Mwenyekiti, Makamu mwenyekiti na Mweka hazina watapatikana kwa kuomba nafasi zao kwa kujaza fomu maalumu, na majina ya waombaji yatachujwa na kamati ya mchujo wa wagombea wakati wa uchaguzi mkuu kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, na majina yao yatawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa Baraza na kupigiwa kura ya siri
iii. Wajumbe wengine wa Bodi ya Uongozi kwa kuzingatia sifa za uongozi zitakazotolewa kwenye kanuni watapatikana kwa kuomba nafasi ya uongozi kupitia majukwaa ya makundi yao ambayo ni
    a. Wanawake
    b. Vijana

Ambapo:

(i) Bodi ya Uongozi itakuwa madarakani kwa miaka mitatu na wajumbe wanaweza kuomba na kuchaguliwa upya kwa kipindi kingine cha pili, na cha mwisho. Hata hivyo mjumbe wa bodi anaweza kuomba nafasi nyingine ya juu ambayo hakuwahi kushika katika vipindi vilivyopita. Endapo miaka mitatu imemalizika,na fedha za kuendesha mkutano mkuu hazikupatikana, basi wajumbe wote wa mkutano mkuu wajigharamie kushiriki mkutano huo.
(ii) Bodi ya Uongozi itafanya kikao kila baada ya miezi mitatu **(3)** na inaweza kuitisha mkutano maalumu wakati wowote litakapojitokeza jambo la lazima kwa manufaa ya Baraza
(iii) Mjumbe yeyote wa Bodi aliyechaguliwa hataruhusiwa kushika nafasi ya uongozi au mtendaji mkuu kwenye Konga au Mtandao kwa kipindi chote atakachokuwa madarakani

6.2.1 Kazi na majukumu ya Bodi ya Uongozi

(i) Kuajiri na kumwajibisha Afisa Mtendaji mkuu kwa kufuata taratibu na kanuni za ajira na kuthibitisha ajira ya watendaji wataalamu wa Baraza

(ii) Bodi ya Uongozi wa baraza itashauri na au kutoa utaratibu, sera na miongozo kwa Sekretarieti katika utekelezaji wa masuala yahusuyo Maendeleo ya Baraza

(iii) Kupitia na kithibitisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Baraza kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Baraza.

(iv) Kupitia na kutathimini bajeti ya mapato na matumizi ya mwaka unaofuata na kuwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa Baraza

(v) Itasimamia mali zote zisizohamishika na madeni na madai ya Baraza

(vi) Itathibitisha iwapo kuna matumizi mabaya ya rasilimali za Baraza au Sekretariati kujiingizia katika vitendo vinavyokwamisha shughuli za Baraza

(vii) Kupendekeza Msikizi (Mkaguzi wa nje wa mahesabu) kutoka taasisi yoyote ya ukaguzi inayotambulika kisheria kwaajili ya kukagua vitabu vya mahesabu ya Baraza.

(viii) Itaunda kamati ndogondogo kama itaona inafaa ili kusaidia utatuzi wa masuala mbali mbali yatakayojitokeza ndani ya Baraza na vyombo vyake

(ix) Kupitia na kuthibitisha dondoo za Mkutano mkuu wa Baraza

6.2.2 Sifa za mjumbe wa Bodi ya Uongozi

(i) Awe na akili timamu

(i) Awe na ari ya kujitolea katika shughuli za Baraza

(ii) Awe Mtanzania wa kuzaliwa

(iii) Awe na umri usiopungua miaka 18.

(iv) Awe anaishi na Virusi vya UKIMWI na yuko wazi isipokuwa nafasi za kitaalamu

(v) Awe na kiwango cha elimu ya msingi na kuendelea kwa nafasi anayoomba au kuteuliwa

(vi) Awe na uwezo wa kuwasiliana na kuwasilisha mada katika ngazi mbalimbali na kutafuta raslimali kwa maendeleo ya Baraza

(vii) Awe na ufahamu kuhusu sera , miongozo na mabadiliko ya hali ya UKIMWI nchini na duniani kwa ujumla

(viii) Awe na uelewa na uwezo wa kutetea misingi ya haki za Binadamu
(ix) Awe na uwezo na sifa za kuongoza.
(x) kwa mujibu wa kifungu cha 6.2.(v) awe na utaalamu unaotakiwa kama vile Usimamizi wa fedha, Utafutaji rasilimali, Utafiti,Ujasiriamali na Sheria.
(xi) Awe mwadilifu na mwaminifu

6.3 Sekretarieti

Kutakuwa na chombo kinachofanya kazi za kila siku za Baraza kiitwacho Sekreterieti, na masuala ya utawala na uendeshaji wa shughuli za Baraza yatatekelezwa na Sekretarieti ya Baraza chini ya Afisa Mtendaji Mkuu

6.3.1 Wajibu na majukumu ya Sekretarieti;

i. Kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Baraza la Watu wanaoishi na VVU
ii. Kupendekeza mipango na mapitio ya kazi zilizofanyika kwenye Bodi ili zithibitishwe na kuidhinishwa na Mkutano mkuu.
iii. Kuhakiki na kusimamia utunzaji wa kumbukumbu na hesabu sahihi za Baraza.
iv. Kuandaa mikutano yote ya Bodi na Baraza.
v. Kuandaa makisio ya Bajeti ya Baraza na kuwasilisha kwenye Bodi ya Uongozi.
vi. Kutoa ushirikiano kwa wakaguzi wa ndani na nje ya Baraza katika ukaguzi wa mahesabu ya baraza.
vii. Kuhakiki makusanyo ya fedha zote zitokanazo na michango na ada za wanachama au utunishaji wa mfuko wa Baraza kwa manufaa ya kuimarisha Baraza.
viii. Sekretariati itaunda idara za utendaji kulingana na mahitaji ya kiutendaji ya Baraza na kuthibitishwa na Bodi

6.4 Konga

Kutakuwa na Konga za Halmashauri za Wilaya, Miji, manispaa na Jiji zitakazoundwa na watu wanaoishi na VVU katika halmashauri husika kwa mujibu wa taratibu na kanuni zitakazowekwa na Katiba ya baraza.

6.4.1 Muundo wa Konga.

Konga itakuwa na muundo ufuatao

(i)Mkutano Mkuu wa Konga

(ii)Kamati ya Utekelezaji

6.4.1.1 Mkutano mkuu wa Konga

Mkutano mkuu wa Konga utakuwa ndicho chombo cha juu kabisa katika Konga (Halmashauri ya Wilaya, mji, manispaa na jiji)

(i) Utaitishwa kila baada ya mwaka mmoja

(ii) Kamati ya utekelezaji inaweza kuitisha Mkutano Mkuu wa Konga au Mkutano mkuu maalum kwa jambo muhimu kufuatana na kanuni na masharti ya katiba hii.

6.4.1.2 Kazi za Mkutano wa Konga

Mkutano huu utafanya kazi na kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kupokea sera na maagizo mbalimbali ya ngazi za juu kwa utekelezaji.

(ii) Kujadili na kutoa maoni juu ya marekebisho ya katiba ya Baraza endapo yatahitajika.

(iii) Kuchagua viongozi wa kamati ya utekelezaji.

(iv) Kuidhinisha na kumuondoa kiongozi yeyote madarakani endapo itathibitika kakiuka katiba na taratibu au kutumia madaraka vibaya,

(v) Kuchagua wawakilishi mbali mbali wa ndani na nje ya Konga **(**mfano CMAC,mkutano mkuu wa Baraza, mikutano au makongamano ya kitaifa na kimataifa)

(vi) Mkutano mkuu wa Konga utachagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti Katibu, Mweka hazina na Wajumbe watano watakaowakilisha watu wanaoishi na VVU katika kamati ya Usimamizi shughuli za Konga. Hii ni pamoja na kuunda kamati ndogo ndogo kwa manufaa na kukidhi mahitaji ya halmashauri husika

6.4.1.3 Wajibu na Majukumu ya Konga za watu wanaoishi na VVU

a. Kuratibu shughuli zote za watu wanaoishi na VVU pamoja na kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali za Watu wanaoishi na VVU

b. Kufanya uraghibishi na utetezi wa masuala ya watu wanaoishi na VVU

c. Kutafuta rasilimali zilizo ndani na nje ya konga zao kwa shughuli za watu wanaoishi na VVU.

d. Kuwahamasisha watu wanaoishi na VVU katika Konga ili wajitokeze kujiunga kwenye vikundi vya kijamii na asasi zisizo za kiserikali za watu wanaoishi na VVU na pia kuwa wazi.
e. Kufuatilia utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI ndani ya halmashauri husika na kutoa ripoti kwa Baraza na Halmashauri husika.
f. Kujenga uwezo wa Uongozi ngazi ya jamii ili kuuwezesha, kuzuia unyanyapaa na ubaguzi
g. Kuimarisha na kuendeleza juhudi za jamii katika kutoa mafunzo, tiba na uegemezi
h. Kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu Dira, Malengo na madhumuni ya Baraza laTaifa la Watu wanaoishi na VVU kupitia semina, warsha na vikundi vya majadiliano katika sehemu zao
i. Kushirikiana na Serikali za mitaa na wadau wengine wenye mwelekeo na mwamko wa kushiriki na kushirikisha watu wanaoishi na VVU kwenye mwitikio wa masuala ya UKIMWI.

Kifungu 7.0: MAJUKUMU NA WAJIBU WA VIONGOZI WA BARAZA.

7.1. MWENYEKITI

Kutakuwa na Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Baraza. Mwenyekiti aliyechaguliwa ataondolewa madarakani na mkutano mkuu wa Baraza kwa mujibu wa katiba hii.

7.1.1 Madaraka na wajibu wa Mwenyekiti

Mwenyekiti aliyechaguliwa chini ya katiba hii atakuwa na madaraka na wajibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo.

i. Kusimamia, kulinda na kutetea Katiba ya Baraza.
ii. Ataongoza vikao vyote vya Baraza isipokuwa vikao vya Sekretarieti.
iii. Kusimamia uongozi kwa kufuata Katiba, na Taratibu zilizowekwa kama vile kuendesha vikao mbalimbali.
iv. Kuhakikisha Baraza linafanikisha malengo na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa katiba.
v. Atakuwa ndiye msemaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU.
vi. Atawakilisha Baraza katika vikao vya nje ya baraza na kutoa mrejesho kwa ajili ya kumbukumbu.
vii. Atakuwepo madarakani kwa muda wa miaka mitatu (3) baada ya hapo anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili, isipokuwa hataruhusiwa kuendelea tena baada ya kipindi cha pili

7.2 Makamu Mwenyekiti

Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano mkuu. Makamu mwenyekiti aliyechaguliwa ataondolewa madarakani na mkutano mkuu kwa mujibu wa Katiba hii na kanuni mbalimbali za Baraza.

7.2.1 Madaraka na wajibu wa Makamu Mwenyekiti

Makamu wa Mwenyekiti aliyechaguliwa chini ya katiba hii atakuwa na Madaraka na wajibu kutekeleza majukumu yafuatayo

i. Kukaimu shughuli zote za Mwenyekiti wakati Mwenyekiti hayupo kwa sababu zozote zile kama inavyoinishwa kwenye katiba hii.

ii. Atakuwa msaidizi na Mshauri Mkuu wa Mwenyekiti katika uendeshaji na Usimamizi wa shughuli za Baraza

iii. Atakaimu nafasi ya Mwenyekiti endapo Mwenyekiti ataacha kuliongoza Baraza kwa mujibu wa Katiba hii. Kipindi cha kukaimu nafasi hiyo hakitazidi miezi sita (6).Baada ya miezi sita, Bodi ya Uongozi itaitisha mkutano mkuu maalumu kwa ajili ya kujaza nafasi hiyo.
iv. Atafanya kazi zozote za Baraza kama atakavyoelekezwa na Mwenyekiti

7.3 Afisa Mtendaji mkuu.

Kutakuwa na Afisa Mtendaji Mkuu ambaye ataajiriwa na Bodi ya Uongozi wa Baraza.Pia Afisa Mtendaji Mkuu aliyeajiriwa ataondolewa madarakani na Bodi ya Uongozi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za ajira za Baraza kulingana na sheria za nchi

7.3.1 Madaraka na wajibu wa Afisa Mtendaji mkuu

Afisa Mtendaji mkuu aliyeajiriwa chini ya Katiba hii atakuwa na madaraka na wajibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo

i. Kuongoza na kuisimamia Sekretarieti ya Baraza
ii. Atakuwa Mratibu Mkuu wa Programu, miradi na Shughuli za Baraza, na atawajibika kwa Bodi ya Uongozi.
iii. Atakuwa Afisa Mhasibu Mkuu wa Baraza na ataidhinisha na kuweka saini katika malipo yote ya Baraza pamoja na Hesabu za Benki
iv. kuandaa mikutano yote ya Baraza kwa mujibu wa katiba kwa maelekezo ya Bodi ya Uongozi.
v. Atakuwa katibu katika vikao vya Baraza na Bodi ya Uongozi isipokuwa Sekretarieti.
vi. Atasimamia na kuongoza Utendaji katika baraza kulingana na Sera, kanuni na taratibu zilizowekwa na katiba hii.
vii. Kuwawajibisha waajiriwa wataalamu wa Baraza na wasaidizi wao kwa mujibu wa kanuni za Baraza na sheria ya nchi, kisha kutoa taarifa kwa Bodi ya uongozi wa baraza
viii. Atafanya na kuratibu mawasiliano yote kati ya Baraza na serikali, taasisi au vyama vingine, mashirika ya kitaifa na kimataifa. Pale itakapobidi, Mtendaji atashauriana na Mwenyekiti na Bodi.
ix. Kufuatilia na Kusimamia masuala yote ya Fedha za Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU na kutoa taarifa kwa Bodi ya Uongozi inapotokea ukiukwaji wa kanuni na taratibu za kiutendaji ndani ya Baraza.
x. Kutekeleza kazi zozote kama atakavyoelekezwa na Bodi ya Uongozi na au Mwenyekiti

7.4 Mweka Hazina.

Kutakuwa na Mweka Hazina ambaye atachaguliwa na mkutano mkuu wa Baraza ambaye ana ujuzi wa utunzaji wa vitabu vya mahesabu na uzoefu katika usimamizi wa fedha.

(i) Atawajibika kwa bodi ya Uongozi kukitokea ukiukwaji wa kanuni na taratibu.

(ii) Kuhakikisha Baraza linafanikisha malengo na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

(iii) Atakuwa mmoja wa watia saini benki kama itakavyoainishwa kwenye kanuni za usimamizi wa fedha za baraza.

(iv) Atatekeleza majukumu mengine kama itakavyoonekana inafaa kwa maslahi ya Baraza.

(v) Ikitokea amekiuka kanuni na taratibu za Baraza, Mweka hazina ataweza kusimamishwa madaraka na Bodi ya Uongozi na hapo kuteua Mweka Hazina wa muda hadi Mkutano wa Baraza Kuu utakapoitishwa na Kujadili hatima yake na au kuteua miongoni mwa wajumbe wa bodi iliyoko madarakani na kuchukua nafasi ya Mweka Hazina kwa mujibu wa Katiba hii. Ikiwa mtu huyo hawezi kupatikana ndani ya bodi basi achaguliwe kutoka ndani ya mitandao na Konga

7.5 Viongozi wa konga

Kutakuwa na viongozi wafuatao wa Konga:-

(i) Mwenyekiti

(ii) Makamu Mwenyekiti

(iii) Katibu

(iv) Mweka Hazina

(v) Wajumbe wanne (wanawake wawili na wanaume wawili)

(vi) Vijana wawili (**me** na **ke**) wanaoishi na VVU

7.5.1 Mwenyekiti wa Konga

Kutakuwa na Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Konga. Mwenyekiti aliyechaguliwa ataondolewa madarakani na Mkutano Mkuu wa Konga kwa mujibu ya katiba hii.

7.5.1a Madaraka na wajibu wa Mwenyekiti wa Konga

(i) Kusimamia,kulinda nakutetea katiba hii.

(ii) Ataongoza Vikao vyote vya Konga

(iii) Atakuwa ndiye msemaji Mkuu wa Konga

(iv) Atawakilisha Konga katika vikao mbalimbali ndani na nje ya Konga.

(v) Atakuwa ndiye mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Taifa la watu wanaoishi na VVU.
(vi) Atachaguliwa kwa kupigiwa kura katika Mkutano Mkuu wa Konga.
(vii) Atakuwepo madarakani kwa muda wa miaka 3,baada ya hapo anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi cha pili isipokuwa hataruhusiwa tena kuendelea baada ya kipindi cha pili kumalizika. Ikiwa Mwenyekiti atakuwa anashika nyadhifa zingine ndani ya mitandao au Baraza basi atalazimika kujiuzuru nafasi hizo
(viii) Mwenyekiti atakuwa ni mmoja wa watia saini kwenye miamala ya benki

7.5.2 Makamu wa Mwenyekiti wa Konga

Kutakuwa na makamu mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Konga.Pia Makamu Mwenyekiti aliyechaguliwa ataondolewa madarakani na Mkutano Mkuu wa Konga kwa mujibu wa katiba hii.

7.5.2a Madaraka na wajibu wa Makamu Mwenyekiti

i. Kukaimu shughuli zote za mwenyekiti wakati mwenyekiti hayupo kwa sababu zozote zile kama inavyoainishwa kwenye kanuni za taratibu za katiba hii
ii. Atakaimu nafasi ya Mwenyekiti endapo Mwenyekiti ataacha kuongoza Konga.Kipindi cha kukaimu nafasi hii hakitazidi miezi 6. Baada ya miezi 6,Kamati ya utekelezaji itaitisha Mkutano Mkuu maalumu kwa ajili ya kujaza nafasi hiyo.

7.5.3 Katibu wa Konga

Kutakuwa na katibu ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Konga na ataondolewa madarakani na Mkutano Mkuu wa Konga.

7.5.3a Madaraka na wajibu wa Katibu wa Konga

(i) Kuongoza na kusimamia shughuli za Konga
(ii) Atakuwa mtendaji na mratibu wa Konga na atawajibika kwa kamati za utekelezaji .
(iii) Atakuwa Afisa Mhasibu Mkuu wa Konga na ataidhinisha malipo.
(iv) Ataitisha na kuandaa mikutano yote ya Konga
(v) Atakuwa katibu wa vikao vyote vya Konga.
(vi) Atasimamia na kuongoza utendaji katika Konga.
(vii) Atakuwa mtia saini katika miamala ya Benki

7.5.4a Madaraka na wajibu wa Mweka hazina wa Konga

Atawajibika kwa kamati ya utekelezaji.

(i) Kukitokea ukiukwaji wa kanuni na taratibu mweka hazina ataweza kusimamishwa madaraka na kamati ya utekelezaji itaweka mweka Hazina wa muda hadi mkutano Mkuu wa utakapopitishwa na kujadili hatima yake

(ii) Mweka hazina atapaswa kuhakikisha Konga inafanikisha malengo yake.

(iii) Atakuwa mmoja wa watia saini katika miamala ya benki

(iv) Mkusanyaji wa michango, Ada na viingilio vya wanachama.

(v) Utayarishaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za Konga.

(vi) Makisio ya Bajeti ya Konga kuwakilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Konga.

(vii) Uandaaji na utunzaji wa kumbukumbu na vitabu vya hesabu za Konga.

(viii) Kuhakiki makusanyo ya fedha zote zitokanazo na Ada ya wanachama au Utunishaji wa Mfuko wa Konga kwa manufaa ya kuimarisha Konga

Kifungu 8.0: Fedha za Baraza.

8.1 Vyanzo Vya Fedha

i. Baraza la watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI litapata fedha kutokana na viingilio na ada ya kila mwaka itakayotolewa na wanachama kupitia kwenye Konga na mitandao
ii. Misaada na zawadi mbalimbali kutoka kwa wahisani, Vyama vya hiari, wadau wa Maendeleo pamoja na michango mingine halali
iii. Ruzuku toka Serikalini na taasisi zingine zinazoshughulikia masuala ya maendeleo kulingana na shughuli za baraza kwa mujibu wa katiba.
iv. Miradi endelevu ya Uwekezaji na Uzalishaji mali itakayo kuwa ikiendeshwa kikamilifu na Watu waishio na VVU.
v. Michango ya hiari kutoka kwa jamii/umma
vi. Utunishaji wa mfuko wa Baraza

Katika kutunza fedha hizo, Baraza la taifa la watu wanaoishi na VVU litamiliki akaunti za benki ambazo moja itakuwa ya fedha za ndani na ya pili itakuwa ya fedha za kigeni kwa kadri itakavyoona kutokana na kukua na umuhimu wa shughuli za Baraza

8.2 Taratibu za Fedha.

Baraza kwa wakati wote litahakikisha linazingatia kanuni na Taratibu za Fedha zilizopo kama zilivyoainishwa katika katiba hii na kama zilivyobainishwa katika sheria ya vyama namba 24 ya mwaka **2002**. Pamoja na yaliyoandikwa hapo juu, Baraza litazingatia utaratibu ufuatao:-

(i) Mhasibu wa Baraza atawajibika kwa Afisa Mtendaji Mkuu
(ii) Masuala yote ya fedha za Baraza yatashughulikiwa na Mhasibu ambaye ataajiriwa na Afisa Mtendaji na kuthibitishwa na Bodi ya Uongozi
(iii) Mwaka wa fedha wa Baraza utaanzia tarehe 1 Julai hadi 30 Juni kila mwaka.=
(iv) Kutakuwa na watia saini wanne **(4)** kwenye akaunti za baraza kwa makundi mawili, yaani kundi A (2) waajiriwa; na kundi B (2) kutoka Bodi ya Uongozi. Saini mbili kwa wakati mmoja, moja kutoka kila kundi moja zitatosheleza uidhinishaji na uchukuaji wa fedha toka kwenye Akaunti ya Baraza.

(v) Mahesabu yote ya mwaka ya Baraza yatathibitishwa na kupitishwa na Bodi ya Uongozi kabla na baada ya kukaguliwa na Mkaguzi wa mahesabu.

8.3 Matumizi ya fedha na Ukaguzi wa Mahesabu ya Baraza.

i. Fedha zote zitatumika kukamilisha malengo ya Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na **VVU**

ii. Shughuli zitakazokasimiwa kutekelezwa zitapendekezwa na Sekretarieti kwenye Bodi ya Uongozi na kupitishwa na wajumbe katika Mkutano Mkuu wa Baraza.

iii. Ukaguzi wa Mahesabu wa Baraza utafanywa na Mkaguzi wa mahesabu anayetambulika kisheria, na aliyepitishwa na mkutano mkuu wa Baraza tu.

iv. Bodi ya Uongozi itateua Mkaguzi wa Mahesabu toka nje na kumwajiri kufanya mahesabu kwa kipindi husika.Malipo kwa ukaguzi yataidhinishwa na Bodi ya Uongozi kwa kuzingatia nafasi na uwezo wa Baraza

Kifungu 9.0. MALI NA DHIMA YA BARAZA

(i) Mali na dhima ya Baraza itaidhinishwa na kuthibitishwa na mkutano mkuu wa Baraza na au mkutano mkuu maalumu wa Baraza. Aidha itatunzwa na kusimamiwa na Bodi ya Uongozi

(ii) Mali zilizonunuliwa na au kuuzwa zitaingizwa katika daftari la mali kwa mujibu wa taratibu

(iii) Mweka hazina ndiye mdhibiti mkuu wa mali na dhima ya Baraza na inapobidi atafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mali kwa maslahi ya Baraza.

(iv) Hakuna mali yeyote na au sehemu yake itakayohamishwa na au kuuzwa bila idhini ya Bodi ya Uongozi inapobidi kwa manufaa ya Baraza.

(v) Bodi ya Uongozi itakuwa na uwezo wa kudai au kudaiwa

(vi) Kwa mujibu wa sheria namba **24 ya mwaka 2002** kuhusu kuweka vitega uchumi kwa fedha za Baraza.Bodi ya Uongozi kwa idhini ya mkutano mkuu wa Baraza,inaweza kuwekeza kama kitega uchumi fedha ambazo ni akiba na hazihitaji kutumika mara moja kwa shughuli za Baraza katika dhamana na vitega uchumi vingine kadri itakavyoona inafaa kwa madhumuni ya kufanikisha malengo ya Baraza.

(vii) Afisa Mtendaji Mkuu ambaye ndiye afisa mhasibu atahakikisha ulipaji na urekebishaji wa madeni yote ya Baraza unafanyika kwa mujibu wa kanuni za baraza.

SURA YA KUMI

10.0. MAREKEBISHO YA KATIBA, USULUHISHI WA MIGOGORO NA KUVUNJWA KWA BARAZA

10.1. MAREKEBISHO YA KATIBA

Marekebisho yoyote ya katiba hii yanaweza kupendekezwa na Bodi ya Uongozi, na au kundi la wajumbe au mjumbe mmoja mmoja wa Mkutano Mkuu wa Baraza, inapoonekana inafaa kwa maslahi na maendeleo ya watu wanaoishi na VVU

10.2 KUVUNJIKA KWA BARAZA LA WATU WANAOISHI NA VVU

(i) Baraza litavunjika kwa mujibu wa katiba hii kwa kuamuliwa hivyo na wajumbe katika Mkutano mkuu wa Baraza na au Mkutano mkuu wa Baraza maalum ikizingatiwa kuwa si chini theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote halali wa mkutano Mkuu waliohudhuria na kupiga kura kupitishia azimio hilo

(ii) Endapo Azimio la kuvunjika kwa Baraza litapitishwa, mkutano mkuu wa Baraza utalazimika kuteua mtu au taasisi inayotambulika kuwa mfilisi wa Baraza baada ya mashauriano na Msajili wa Vyama.Aidha mkutano mkuu utaandaa taratibu za mgawanyo wa mali na madeni ya Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU

(iii) Baada ya utekelezaji wa kifungu 10.0 mali ya baraza iliyobaki baada ya kulipa madeni itapelekwa kwenye taasisi inayofanya kazi sawa na Baraza na yenye malengo na madhumuni sawa na Baraza.

10.3 . USULUHISHI WA MIGOGORO YA NDANI YA BARAZA

Migogoro yote inayohusu shughuli na masuala ya Baraza itashughulikiwa kupitia vyombo vilivyowekwa na katiba hii katika ngazi husika ndani ya baraza tu. Mwanachama anayo haki na wajibu wa kutoa dukuduku lake kupitia taratibu na kanuni zilizowekwa na baraza ama katika kusikiliza, kusikilizwa na au kutoa maoni yake kwa vyombo husika. Ikiwa hataridhika na maamuzi yaliyotolewa anaruhusiwa kukata rufaa kwa ngazi ya juu ya Vyombo vya baraza.

Kifungu 11.0 : MAELEZO MENGINEYO

Baraza hili linaundwa na Watu wanaoishi na VVU kwa hiari yao chini ya sheria ya Tanzania, Sheria Namba **24 ya mwaka 2002** ya Vyama (Asasi zisizo za Kiserikali) vya hiari na uendeshaji wake utakuwa katika misingi ya Sheria za Tanzania.

Katiba hii itaanza kutumika baada ya kupitishwa kwa kuungwa mkono na ¾ ya wajumbe halali waliohudhuria mkutano mkuu wa Baraza.

11.1. MUHURI NA NEMBO YA BARAZA

Muhuri wa Baraza utabandikwa katika nyaraka muhimu zilizothibitika kuwa na manufaa kwa Baraza la watu wanaoishi na VVU. Muhuri wa Baraza utatunzwa na Afisa Mtendaji Mkuu katika Makao Makuu ya Baraza. Kutakuwa na Muhuri wa Baraza utakaokuwa na maneno yafuatayo :-

The National Council of People Living with HIV&AIDS'' (NACOPHA) REG. NO 13269 P.O.BOX 55811 DAR ES SALAAM

11.2 NEMBO YA BARAZA

Kutakuwa na **'NEMBO''** ya Baraza itakayoonekana katika Nyaraka na maandishi yote ya Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na **VVU**.

12.0 : Marekebisho ya katiba ya NACOPHA ya mwaka 2005

12.1 : Baada ya kupitishwa na kuanza kutumika marekebisho haya, katiba ya NACOPHA ya mwaka 2005 inarekebishwa kwa masharti yaliyowekwa katika marekebisho haya.

Imetayarishwa na Kuwasilishwa na viongozi wa NACOPHA mbele yangu leo tarehe Mwaka Elfu mbili na kumi na tatu (2013)

S/N	Jina	Cheo	Sahihi
1	Vitalis Vitus Makayula	Mwenyekiti	
2	Deo Crispin Mlori	Makamu Mwenyekiti	
3	Mitterand Mohamed Dagila	Mweka Hazina	
4	Asia Adam	Mjumbe	
5	Justice Mboya	Mjumbe	
6	Francis Stola	Mjumbe	
7	Stigmata Tenga	Mjumbe	

Baraza la Taifa la watu wanaoishi na VVU' (NACOPHA)
S.L.P 55811 Dar es Salaam ; Tanzania
Simu +255 22 2701210
Nukushi. +255 22 2701209
Barua pepe: nacopha@nacopha.or.tz,
Tovuti www.nacopha .or.tz